



KENYA BANKERS
ASSOCIATION

ILANI KWA UMMA

Tarehe ya kutolewa: Oktoba 14, 2015

Kuambatana na taarifa iliyotolewa kwa umma na Benki Kuu ya Kenya mnamo Oktoba 13, 2015 kuhusu uteuzi wa shirika la Kenya Deposit Insurance (KDIC) kuchukua usimamizi na udhibiti wa Benki ya Imperial Bank Limited, Halmashauri ya kusimamia sekta ya benki nchini (KBA) ingependa kutoa habari zaidi kuhusiana na suala hili.

HATUA ZA MAPEMA ZILIZOCHUKULIWA NA WAHUSIKA WOTE

- Kulingana na taarifa zilizotolewa na Benki Kuu ya Kenya (CBK), Bodi ya wakurugenzi ya benki ya Imperial Bank Limited hatua za moja kwa moja za marekebisho zilizohitaji kuchukuliwa na CBK. CBK pia ilitoa majibu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Capital Markets Authority na Benki ya Uganda, na kuhusu matokeo ya baadaye katika sekta ya fedha.
- Katika taarifa iliyotolewa na mdhibiti, ufichuzi huo wa Bodi ya Benki ya Imperial ulikaribishwa kwani uliwezesha CBK kutoa majibu thabiti. Kutokana na hatua hii, CBK ilitokeleza mamlaka yake kisheria na kutekeleza wajibu wa kulinda wema wa umma ili kulinda maslahi ya wawekaji amana na wawia wa Benki ya Imperial Bank Limited.

SEKTA YA BENKI NCHINI KENYA INASALIA SALAMA NA THABITI

- CBK na KBA zimehakikishia umma kuwa sekta ya benki nchini inasalia salama na thabiti.
- KBA imejitolea kufanya kazi na CBK kuhakikisha kutolewa kwa usaidizi na taarifa zinazofaa kwa sekta ya benki ili kuzuia fununu ambazo huenda zikaathiri imani ya soko. Haya yakijiri, CBK imejitolea kutumia ala ilizo nazo kutoa usaidizi wa kulipa madeni kwa mfumo wa benki kuhakikisha uthabiti wake wakati huu.

TATIZO LINALOKUMBA BENKI YA IMPERIAL NI LA KIPEKEE NA SIO LA KIMFUMO

- Kampuni ya Benki ya Imperial Bank inawakilisha asilimia 1.8 ya sekta ya benki, na ni maoni yetu kama KBA kuwa tukio hili halipaswi kuibua wasi wasi katika sekta hii.
- Hatua ya kuteuliwa kwa KDIC kuchukua usimamizi wa benki hii inanuiwa kutoa jukwaa kwa KDIC kutekeleza mamlaka yake ya kisheria kama usaidizi kwa bodi ya wakurugenzi wa Benki ya Imperial Bank Limited katika harakati za kurejesha usalama na uthabiti wa benki hii.

TAHADHARI KUHUSU TAARIFA ZA UWONGO NA UVUMI

- Kuna taarifa za uwongo zinazoenea kwenye mtandao wa kijamii zinazodai kutambua orodha ya benki ambazo zimeshindwa kutimiza “viwango fulani”. CBK kwenye taarifa iliyotolewa Oktoba 14, 2015 ilihakikishia soko la kifedha na umma kuwa taarifa na madai haya ni ya uwongo.
- Kama KBA, tunashauri dhidi ya usambazaji wa uvumi huu wa kuchafua jina kuhusu benki fulani. Tunaomba wateja wa benki kuwasilisha maoni yao moja kwa moja kwa benki zao au katika Idara ya Ukaguzi wa Benki ya CBK.

KDIC ITAWAONGOZA WAWEKAJI AMANA KUHUSU MWELEKEO

- KDIC imetoa mawasiliano kuhusu usimamizi wa Benki ya Imperial na itazidi kuwapa wateja wa Benki ya Imperial ripoti za hatua zilizochukuliwa.
- Kwa maswali kuhusu Benki ya Imperial, tafadhali wasiliana na KDIC wakati rasmi wa kazi, Jumatatu hadi Ijumaa – saa mbili unusu asubuhi hadi saa kumi unusu alasiri, kwa simu nambari 0770887992/2863813 au kupitia barua pepe: customerservice@depositinsurance.go.ke.
- Kuhusu maswali mengine kuhusu benki, wateja, washika dau na wafanyakazi wanapaswa kuwasiliana na Idara ya mawasiliano ya benki hiyo au kitengo cha wateja.

BENKI ZINA WAJIBU WA KUWAELIMISHA WATEJA

- Sekta ya benki nchini Kenya inaongoza barani Afrika kwa misingi ya ujumuishaji na ufikiaji wa huduma rasmi za benki. Kutokana na hayo tunatambua kuwa benki zina wajibu wa kuhakikisha kuwa wateja wake wanaelimishwa kuhusu manufaa na hatari za bidhaa na huduma wanazotoa, vile vile viwango vya shughuli bora za benki kuambatana na KBA kwenye “Mwongozo wa Sekta ya Benki ya Kenya kwa Wateja”.
- Benki zina wajibu mkuu wa kuwafahamisha wawekaji amana na wenye hisa kuhusu miundo ya uongozi, sera na usimamizi jumla wa taasisi hizi kuambatana na miongozo ya utaratibu wa CBK.
- Kwa hivyo Afisi ya KBA inahimiza benki abazo ni wanachama wa KBA kuendelea kuwaelimisha washika dau wao kuhusu suala hili, vile vile kutoa taarifa na huduma kwa wateja ili kuangazia masuala yanayokumbwa wateja wao.

Muungano wa Benki wa Kenya ungependa kuwahakikishia wanachama wake na umma kuwa ukuaji na uthabiti unaozidi kushuhudiwa katika sekta ya benki nchini ni thabiti kupitia usimamizi na udhibiti katika mazingira yanyofaa.

Tafadhali tembelea www.kba.co.ke na www.centralbank.go.ke kwa maelezo zaidi ya wateja kuhusu sekta ya benki nchini.